**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia uzima na Afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukue fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii adhimu na muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita kwa umahiri wake na umakini wa hali ya juu aliouonesha kila wakati Kamati ilipokutana na Wizara hii. Shukurani za kipekee tunazitoa kwake kwa ushirikiano mkubwa aliotupatia katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Vile vile, tunatoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu Ndugu. Fatma Hamad

Rajab na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Kamati hususan katika kupitia bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**Mheshimiwa Spika,**

Shukurani za pekee nazitoa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa ujasiri wao waliouonesha katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2021/2022 na hatimaye kuipitisha bajeti hiyo pamoja na marekebisho madogo madogo waliyoyafanya kwa nia ya kuimarisha zaidi utendaji wa Wizara. Kwa heshima kubwa napenda kuwatambulisha Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

1. Mheshimiwa Yahya Rashid Abdallah - Mwenyekiti
2. Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis - M/Mwenyekiti
3. Mheshimiwa Abdalla Abbasi Wadi - Mjumbe
4. Mheshimiwa Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
5. Mheshimiwa Haji Omar Kheir - Mjumbe
6. Mheshimiwa Zawadi Amour Nassor - Mjumbe
7. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
8. Ndugu Mussa Issa Mussa - Katibu
9. Ndugu Azmina Hamad Khamis - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**

Jadweli la kwanza ambalo limeundwa chini ya Kanuni ya 106 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, inazitaka Kamati za kisekta kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka. Katika utekelezaji wa matakwa ya Kanuni hiyo, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilitekeleza wajibu wake kwa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo mnano tarehe 02/05/2021 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya Maelezo hayo, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Ustawi ya Jamii naomba niwasilishe mbele ya Baraza Lako Tukufu Maoni ya Kamati yangu kuhusiana na Bajeti hiyo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Programu Kuu hii, Kamati yangu itajikita zaidi katika kuzungumzia changamoto tulizozibaini katika utekelezaji na usimamizi usiorizisha katika Programu ndogo zote mbili zilizo chini ya utekelezaji wa Programu Kuu hii.

## PROGRAMU NDOGO YA UPATIKANAJI NA USAMBAZAJI WA HABARI

**Mheshimiwa Spika,**

Kama inavyofahamika, Programu ndogo hii inatekelezwa kupitia Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Utangazaji Zanzibar, Shirika la Magazeti pamoja na Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imegundua Shirika la Magazeti la Zanzibar linakabiliwa na changamoto kubwa ya madeni wanayodai kwa Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaowapelekea huduma hii ya magazeti, hivyo hulibebesha Shirika letu mzigo mkubwa wa madeni ya Uchapaji ambapo hadi tunaiwasilisha taarifa hii katika Baraza hili tukufu Shirika la Magazeti linadaiwa **shilingi 227,000,000 (Milioni Mia Mbili na Ishirini na Saba)** na Wakala wa Serikali wa Uchapaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamadunu na Michezo kuandaa utaratibu wa kuzitaka moja kwa moja fedha za Matumizi mengineo ya Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinazodaiwa na Shirika la Magazeti ili kuweza kulisaidia Shirika kuweza kujiendesha  na kutoa gawio stahiki na kuinua uchumi wa Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kukiimarisha Kitengo cha Masoko cha Shirika hili Magazeti yetu yaweze kuwafikia wananchi kwa haraka na kusomwa na watu wengi wa Zanzibar na Tanzania Bara kwa ujumla kwani Kamati imebaini usambazaji na utoaji wa Gazeti la Zanzibar Leo hauridhishi kutokana na kukosekana kwa masoko ya uhakika ndani ya Tanzania hali inayopelekea Shirika kuzalisha magazeti, lakini mengi yanabakia ofisini kwa kukosa soko.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri magazeti kusambazwa hadi vijijini na sio mjini pekee, ikiwemo vijiji vya Nungwi, Makunduchi, Micheweni na Mkoani, yaani Zanzibar nzima.

## PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA VYOMBO VYA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Programu ndogo hii Kamati itajikita zaidi katika huduma inayotolewa ya Usimamizi wa Shughuli za Uchapaji kama inavyoeleweka Serikali iliyopita ya Awamu ya Saba iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Mpendwa Mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein ilichukuwa juhudi kubwa za kuhakikisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji unaimarika kwa kuboreshwa  kwa kujengewa majengo ya kisasa pamoja na kununua mashine mpya na mitambo yakisasa ili waweze kujiendesha kibiashara na kuongeza pato la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya juhudi hizo zilizochukuliwana Serikali, Kamati imebaini utendaji wa Wakala wa Uchapaji wa Serikali bado unasuasua katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku na kupelekea kukumbwa na changamoto mbali mbali zinazoikosesha Serikali mapato.

**Mheshimiwa Spika,**

Uwepo wa madeni makubwa na ya muda mrefu ya wafanyakazi wa ndani yanayotokana na malimbikizo ya malipo ya muda wa kazi wa ziada 'Overtime' ambapo takriban hadi sasa yamefikia Bilioni 1.8.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia imegundua kuwa madeni haya yametokana na ukiukwaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Namba 2 ya Mwaka 2011 na hivyo kupelekea madeni hayo kufikia kiwango kikubwa kisichoridhisha kwa Serikali. Kwa mujibu wa Kifungu cha 57(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2014 inaelekeza mfanyakazi yoyote anastahiki kudai fedha za muda wa ziada wa kufanya kazi kwa muda usiozidi masaa 3, ila deni hili tunalolizungumzia hapa wapo wafanyakazi wanaodai fedha za muda wa ziada kwa masaa ishirini kwa siku jambo ambalo sio sahihi na ni kinyume na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa Mnasaba huo, Kamati inaiomba Serikali kwa Kushirikiana na Wizara ya Habari kulishughulikia suala hili kwa kufanya rejea ya malipo na kumbukumbu zote za nyuma za madai ili kutambua changamoto iliopo na nani anayestahiki kulipwa kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kipindi kirefu hivi sasa ZAGPA imeshindwa kufanyakazi kwa ufanisi kutokana na ukosefu wa fedha unaochangia kuwepo kwa madeni makubwa ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadhi ya Mashirika ya watu binafsi wanaopeleka kazi zao kwa Wakala huo na kushindwa kulipa madeni yao kunakopelekea Wakala kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na kadhia ya madeni makubwa yanayoikumba Wakala kwa utoaji wa huduma tunaiomba tena Serikali yetu Sikivu inayoongozwa na Jemedari wetu Mhe. Rais Hussein Ali Mwinyi kuzitaka taasisi zote zinazodaiwa na Wakala kulipa madeni hayo haraka kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara, kwani kufanya hivi ni kuisaidia Wakala kuondokana na ukakasi wa matumizi wakati fedha za kutosha ziko mikononi mwa taasisi mbali mbali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Changamoto nyengine inayopelekea kuzorota kwa kazi ni kuchelewa kufanyiwa 'Service' kwa muda unaohitajika kwa Mashine na Mitambo inayotumika katika utekelezaji wa kazi zao za Wakala wa Uchapaji hali hiyo hurudisha nyuma ufanisi wa Wakala huo na hatimaye kusababisha kuharibika mara kwa mara mashine na mitambo hiyo,

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inayo taarifa kuwa kuna baadhi ya mitambo iliopo ndani ya Wakala huo imeshafanya kazi kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa 'Service' yoyote kwa miaka mingi

sasa ikiwemo mitambo mipya ilifungwa katika Serikali ya awamu ya Saba mitambo ambayo iligharimu fedha nyingi za Serikali katika ununuzi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaishauri Serikali katika kuitafutia ufumbuzi unaofaa changamoto hii ya uharibifu wa Mashine ili kuweza Wakala wa Uchapaji wa Serikali kufanya kazi zake kiufanisi zaidi na kitaalamu. Kamati, inaona ipo haja ya fedha iliotengwa katika Fungu la Fedha za Miradi ya Maendeleo katika Huduma ya HJ03010103 kwa ajili ya utekelezaji wa Ununuzi wa Mtambo Mpya wa Kuchapia Magazeti wenye thamani ya **Tshs. 13,747, 481,000 (Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Saba na Arubaini na Saba, Lakini Nne na Elfu Thamanini na Moja)** kuzielekeza kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji, kwani hata hilo gazeti nalo linachapwa huko.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali imeweka Bohari kwa lengo la kutoa huduma za vifaa kwa taasisi za Serikali. Jambo la kusikitisha Bohari hii haitumiki kwa matumizi ya vifaa vya maofisi ya Serikali, ambapo kiuhalisia Ofisi zetu nyingi zinapohitaji vifaa vya kuandikia 'Stationaries' hutumia sana fedha za Serikali kwenda katika maduka yanayomilikiwa na watu Binafsi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaiomba Serikali kuendelea, kusimamia na kusisitiza kwa taasisi zote za Serikali kununua vifaa vya kuandikia kwa maana ya 'Stationaries' wakanunuwe katika Bohari yetu ya Serikali, ili kuiwezesha kimapato kama taasisi za Serikali zinavyoelekezwa kuchapisha kazi zao katika Wakala wa Serikali wa Uchapaji. Jambo ambalo halifanyiki kwa taasisi nyingi za Serikali.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inatekelezwa na Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana ambayo ni **SJ030201.** Dhumuni kuu la kuanzishwa kwake ni kuwawezesha Vijana ili kujenga uzalendo, kupanua demokrasia, kukuza uchumi na maendeleo ya Vijana. Programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa kazi kubwa iliyofanyika katika kuhakikisha tunakuza vipaji vya vijana wetu ili waweze kuajiriwa na kujiajiri wenyewe Serikali ilitenga fedha Milioni 565 kwa ajili ya kujenga 'Green House' 19 kwa Unguja na pemba kwa kila Wilaya.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, matokeo ya Mradi huu wa Ujenzi wa 'Green House' hizo manufaa yake hayakuwa chanya kwa vijana waliokusudiwa kutokana na mradi huu kukumbwa na hitilafu nyingi za kiutendaji ikiwemo ukiukwaji wa mkataba, Ukosefu wa ushirikishwaji kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika utekelezaji wa mradi kama mkataba unayoelekeza, kutofanyika upembuzi yakinifu katika maeneo yote ya Unguja na Pemba yaliokusudiwa Miradi hiyo kujengwa (Feasibility Study), kuipa kazi ya Ujenzi pamoja na Uchimbaji wa Visima Kampuni ya Kikosi cha Kujenga Uchumi Zanzibar(JKU) ambayo haina uwezo wa kazi hizo, kukosekana kwa Ushirikishwa wa Mamlaka ya Maji Zawa katika Uchimbaji wa Visima hivyo na kutowashirikisha Vijana wenyewe katika hatua za awali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na mapungufu hayo niliyoyataja hapo juu ya Utekelzaji wa Mradi huo hatimaye azma na malengo ya Serikali kutokufikiwa hususan ya kuinua kipato cha Vijana wetu kwa waliokusudiwa katika jamii zetu kwa kuwapatia ajira itakayowainuwa uchumi wao ili waweze kujitegemea angalau kujitatulia changamoto za kupata mahitaji yao muhimu ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia imebaini ndani ya mradi huu kuna udanganyifu wa fedha za Serikali umefanyika kwani Kamati hii ilipofika katika baadhi ya maeneo iliopo 'Green House' hizo imekuta hakuna chochote kilichofanyika zaidi ya kujenga mabanda tu. Pamoja na sababu zote hizo Kamati inasema wazi haikuridhishwa na utekelezaji wa Mradi huu tangu katika hatua ya awali ya Usimamizi ambapo Baraza la Vijana na Idara ya Maendeleo ya Vijana ndio wasimamizi wakuu wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Hali hii imewakosesha matumaini na imani kwa vijana wetu ambao ndio Taifa la kesho kutokana na usimamizi usiokuwa na ufuatiliaji wa wahusika wakuu hali iliyopelekea Kampuni kulipwa fedha zote za Ujenzi ambapo hadi saa kazi hazijakamilika na mkataba umeshamaliza muda wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na kasoro zilizojitokeza katika mradi huu, Kamati inaiomba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kukaa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuzungumzia jambo hili ambapo fedha nyingi ya Serikali

imeelekezwa bila ya mafanikio wakati wahusika bado wapo katika kusubiria mradi huo ambao ni muokozi na tegemeo lao.

**Mheshimiwa Spika,**

Juhudi kubwa imeshapita kwa Wizara ya Habari kulitafutia ufumbuzi jambo hili bila ya kupata majibu wala mashirikiano hadi hivi sasa kutoka kwa wakandarasi wa Kikosi cha Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU).

**Mheshimiwa Spika,**

Kukosekana kwa majibu hayo, Kamati inaitaka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia Kikosi cha Kujenga Uchumi (JKU) kuzirudisha fedha hizo walizolipwa kwa ajili ya kazi ya Uchimbaji wa Visima kwenye Mradi wa Green House 19, ambayo imewashinda kutekeleza.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika bajeti hii mpya ya mwaka 2021/2022 kuna Tshs. 7,000,000,000 bilioni pia zinazoelekezwa katika kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Vijana. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara kusimamia vyema matumizi ya fedha hizo ili yasijekujitokeza tena yaliokwisha kujitokeza huko nyuma. Aidha, Kamati inashauri fedha hizi zipelekwe kwenye miradi ambayo imeshafanyiwa utafiti na ambayo inatokana na mahitaji ya vijana wenyewe.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa kazi zake imebaini katika Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti kuna mapungufu makubwa ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba wanaoingia na wakandarasi wa Ujenzi ambapo katika Wizara hii takribani miradi yote ya Maendeleo iliyokuwa ikitekelezwa inasuasua hususan katika suala la matumizi ya fedha zilizotengwa kwa mradi husika mfano halisi wa miradi hiyo:

- Kutokamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la ZBC Pemba ambapo mkataba ushamaliza na jengo bado halijakamilika hadi tunawasilisha taarifa hii Mradi huu ulikabidhiwa Chuo cha Mafunzo ambapo kwa taarifa tulizopokea bado Mkandarasi wa Ujenzi anaidai Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.
- Kutokamilika kwa baadhi ya Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo vilivyokusudiwa kujengwa kwa kila Wilaya kwa Unguja na Pemba ambapo Kamati imegundua kuna ukiukwaji wa mkataba katika mradi huu na kupelekea kulipwa Wakala wa Barabara (UUB) Tshs. 254,193,800.00 (Milioni Mia Mbili na Hamsini na Nne, Laki Moja na Tisiini na Tatu na Mia Nane) Milioni kinyume na utaratibu wa Sheria.
- Kutokamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa ‘Green House’ 19 zilizokusudiwa kujenga kila Wilaya kwa Unguja na Pemba kama tulivyoelezea hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaiomba Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Tafiti za Wizara kwa kushirikiana na Viongozi wa Wizara hii kuwa mstari wa mbele katika kulinda matumizi

ya fedha na kuwa imara pia katika usimamizi wa mikataba wanayoingia katika utekelezaji wa miradi wanayoisimamia**.**

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA AFISI KUU PEMBA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu haijaridhishwa na kiwango cha makusanyo ya Mapato kilichopangwa kwa Afisi Kuu Pemba kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kwani Kamati imegundua kuna vyanzo vingi Pemba vya makusanyo ya Mapato hayo lakini makadirio yaliowekwa mwaka huu ni madogo sana.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kukaa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuangalia vyanzo vyengine vya mapato, ambavyo hapo awali wameviacha na vinaweza kuchangia pato la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa umakini na usikivu wao wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kwa vile Kamati ya Ustawi wa Jamii imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, na Michezo naomba sasa nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kuichangia, kuijadili, kuhoji na hatimaye kuipitisha bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana na Michezo kwa mwaka wa Fedha wa 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo, Kwa niaba Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na wananchi wa Jimbo la Konde naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………..
Mhe. Zawadi Amour Nassor,
Mjumbe
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**